Stanbic Bank

# MAELEZO NA MASHARTI YA UFUNGUAJI WA AKAUNTI YA BINAFSI

## 1. Utangulizi

1.1 Hati hii ina Masharti kwa Bidhaa na Huduma zetu isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo katika Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma. Pamoja na Masharti haya kila Bidhaa na Huduma zetu zina maelezo na masharti ambayo ni mahsusi kwa Bidhaa/ Huduma inayohusika (Masharti Maalum ya Bidhaa/Huduma).

1.2 Masharti haya na Masharti Mahsusi mengine ya Bidhaa na Huduma yanafanya mkataba baina yako na sisi, kwa hiyo tafadhali hakikisha unayaelewa yote.

1.3 Ibara muhimu ambazo zinaweza kuondoa uwajibikaji wetu au zinahusu hatari zitaandikwa kwa wino mzito au msisitizo. Sharti uzingatie vizuri ibara hizi.

1.4 Kumbuka kwamba siku zote sharti utimize Masharti haya.

## 2. Tafsiri

Tumetafsiri baadhi ya maneno kwa ajili ya usawa Maneno haya yataanza na herufi kubwa, pale itakapoelezwa. Neno moja hujumlisha wingi na kinyume chake.

**"Misimbo ya Matumizi"** ina maana ya misimbo yoyote ya siri (herufi na tarakimu) unaotumia kupata Matumizi ya Bidhaa na Huduma Pamoja, kwa mfano: namba ya Kadi Yako, utambulisho wa kidigitali PINI, jina linalotumika na nywila inayotumika.

**"Akaunti"** ina maana ya Akaunti ya benki iliyofunguliwa na Sisi kwa jina lako kwa maombi yako.

**"Kadi ya Ziada"** ina maana ya Kadi yoyote ya ziada iliyounganishwa na Akaunti yako.

**"Mmiliki ziada wa Kadi"** ina maana ya mtu ambaye tunamkabidhi Kadi ya ziada baada ya maombi yako, mathalan mwenza, mshirika, mtoto au mfanyakazi.

**"Mkataba"** ina maana Fomu ya maombi iliyoambatishwa na kusomwa pamoja na maelezo haya na Maelezo na Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma.

**"Mshirika"** ina maana ya kampuni Tanzu au Kampuni Kuu.

**"ATM"** ina maana ya Mashine ya Kutoa Fedha Inayojiendesha.

**"Chombo chenye"** ina maana ya mamlaka ya serikali au nyingine ambayo imeidhinishwa kufanya usimamizi au mamlaka ya utekelezaji sheria kwa Benki au wewe.

**"Siku ya Kazi"** ina maana ya siku yoyote ambayo kwa kawaida kazi hufanyika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiachia Jumamosi, Jumapili na sikukuu za umma.

**"Kadi"** ina maana Kadi yoyote ya Benki tunayotoa kwako kwa ajili ya Akaunti yako pamoja na Kadi ya Ziada au kadi mbadala.

**"CDM"** ina maana ya mashine ya kuingiza fedha.

**"Msimbo"** ina maana ya Msimbo wa Hazinaya Marekani wa mwaka 1896( kama unavyorekebishwa mara kwa mara).

**"FACTA"** ina maana ya Sheria ya Utekelezaji Kodi wa Akaunti za Kigeni (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara).

**"Kundi"** ina maana ya Standard Bank Group Limited na kila Mshirika wake.

**"Kampuni Kuu"** ina maana ya kampuni iliyo juu ya kampuni zake tanzu.

**"HATI"** ina maana ya kitu chochote kama vile kitabu cha hundi au kadi kwa ajili ya Matumizi ya Akaunti yako.

**"IRS"** ina maana ya Huduma ya Hazina ya Ndani ya Marekani (kadiri inavyorekebishwa mara kwa mara).

**"Sheria"** ina maana ya sheria, kanuni, hukumu, na amri za mahakama yoyote yenye mamlaka, Benki Kuu au wakala wa serikali au mamlaka

yenye nguvu ya kisheria katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au mamlaka yoyote inayohusika.

**“Mfanyabiashara”** ina maana ya mtoaji bidhaa au huduma.

**“Taasisi ya Fedha Isiyo Mshirika”** ina maana iliyoainishwa kwenye Msimbo.

**“Tumia”** ina maana ya uendeshaji wa Akaunti yako na Utekelezaji na Utendaji vina maana mmoja.

**“Taarifa Binafsi“** ina maana ya Taarifa kuhusu mtu halisi anayetambulika na au pale inabidi, mtu kisheria, pamoja na, lakini sio pekee, taarifa kuhusu mbari, jinsia, mimba, hadhi kindoa, utaifa, rangi, umri, hali ya kimwili au akili, uwezo kimali; athari, dini, imani, utamaduni, lugha, uzawa, elimu, kitabibu,kifedha, historia ya kijamii au ajira, namba yoyote ya utambuzi, alama, barua pepe, anuani ya posta au ya mahali, namba ya simu, eneo, kitambulisho chochote cha kimawasiliano, kazi nyingine yoyote ya mhusika, taarifa kuhusiana na Akaunti, maoni binafsi, maoni au utashi wa mhusika au maoni au utashi wa mtu mwingine mintarafu mhusika, mawasiliano yaliyotumwa na mhusika ambayo dhahiri au kiufahamifu yana silka ya kibinafsi au siri, au mawasiliano ya awali, na jina la mtu iwapo linawezekana kuwa na taarifa nyingine kuhusu mtu huyo au iwapo kufichuliwa kwa jina lenyewe kutaonyesha taarifa ya mtu huyo.

**“PINI”** ina maana ya namba ya siri ya utambulisho wa mtu inayotumika kwenye Akaunti yako, pamoja na PINI iliyochaguliwa na mteja.

**“POS”** Mashine ya kielekroniti kwaajili ya malipo kwa kutumia Kadi ya Benki.

**“Mchakato”** ina maana ya matumizi au kitendo chochote kinachojiendesha au la kuhusu Taarifa Binafsi, pamoja na: mabadiliko, uzuiaji, urekebishaji, ukusanyaji, ushauri, ushushaji, uharibifu, utoaji taarifa kwa njia ya usambazaji, au kufanya ipatikane kwa namna yoyote, ufutaji, uunganishaji, upangaji, upokeaji, kurekodi, kuchukua, kuhifadhi, kuboresha, kurekebisha au matumizi ya taarifa. Utumiaji na Iliyotumika itakuwa na maana moja.

**“Bidhaa”** ina maana ya aina mbalimbali za akaunti zisizo na miamala ya mikopo pamoja na akaunti za akiba na uwekezaji tunazozitoa kwa wateja wetu pamoja na huduma zinazohusiana na Akaunti. Huduma ina maana kama hiyo.

**“Akaunti”** ina maana ya Akaunti na Marekani ambayo haijatoa nyaraka zozote zilizotakiwa kuthibitisha umiliki wa mwenye Akaunti ya hadhi ya FATCA au daraja hilo.

**“Kanuni”** ina maana ya kanuni yoyote, amri ya kiofisi, maelekezo au muongozo (uwe na nguvu ya kisheria au la) au amri yoyote ambayo Benki imechagua na/au inawajibika kuitekeleza na/au iko kwa mujibu wa taratibu za benki yenye hadhi (katika upekee na hiari yake) ya serikali yoyote, serikali shirikishi, chombo cha kimataifa, wakala au idara au chombo cha udhibiti, mamlaka au shirika jingine. (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara).

**“Mtu”** ina maana ya mtu (halisi au kisheria) ambaye amezuiliwa na Mamlaka ya Uwekaji Vikwazo.

**“Mamlaka”** ina maana moja au muungano wa asasi zifuatazo;
Ofisi ya Udhibiti wa Mali za Kigeni za Idara ya Hazina ya Muungano wa Mataifa ya Marekani, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya, Hazina ya Malkia, Wizara ya Uchumi, Fedha na Viwanda ya Ufaransa na mamlaka inayotambuliwa na sisi mara kwa mara.

**“Benki ya Stanbic au Sisi”** ina maana ya Benki ya Stanbic Tanzania (Namba ya Usajili 22443), Kampuni ya Marekani iliyosajiliwa rasmi kwa dhima ya ukomo kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Na.12 ya 2002, Tanzania Bara na kupewa leseni chini ya Sheria ya Taasisi za Benki na Fedha, 2006 (Sheria Na.5 ya 2006) kama ilivyorekebishwa na/au warithi wa mali au wahawilishiwa.

**“Chanzo Mapato”** ina maana ya mapato yasiyo badilika au yanayobadilika kwa mwaka au nyakati kutoka mapato ndani ya Marekani kama inavyoainishwa na FATCA, kanuni ya hazina ya Marekani 1.1473- 1(a)(2). Wakala Mdhibiti maana yake ni taasisi ya fedha au benki yenye

Stanbic Bank

mamlaka ya kudhibiti Chanzo cha Mapato ya Marekani kwa mujibu wa mkataba na Marekani.

**"Kampuni Tanzu"** ina maana ya chombo ambacho mtu ana udhibiti wa moja kwa moja au anamiliki moja kwa moja au sio moja kwa moja au sio moja kwa moja zaidi ya 50% (asilimia hamsini) ya mtaji wa kupiga kura au haki kama hiyo ya umiliki na udhibiti. Kwa muktadha huu umiliki na udhibiti ina maana ya uwezo wa kuelekeza utawala na sera za chombo ama kupitia umiliki wa mtaji wa upigaji kura, kwa mkataba au vinginevyo. Kampuni itachukuliwa kama mjumbe wa kampuni tanzu ikiwa hisa zake zimesajiliwa kwa jina la:

(i) Mteule; au

(ii) Mhusika yeyote mwenye usalama kwenye hisa hizo au mteule wa mhusika

**"Muamala"** ina maana ya makato au nyongeza yoyote kwenye Akaunti yako yaliyofanywa iwe au isiwe Hati, PINI au kifaa kimetumika. Inajumlisha malipo yoyote ya bidhaa au huduma, kuweka, kutoa au kuhawilisha fedha au thamani. Fanya na Ufanyaji vina maana moja.

**"US"** ina maana ya Muungano wa Mataifa ya Marekani

**"Akaunti ya Marekani"** ina maana akaunti inayomilikiwa na raia wa Marekani, mlipa kodi mkazi wa Marekani au akaunti yenye mmiliki wa Marekani ambaye ni mtu aliyeainishwa na FATCA.

**"Mdhibiti/ Wakala wa kizuizi"** ina maana yake ni taasisi ya fedha au benki iliyozeshwa na Muungano wa Mataifa ya Marekani kuzuia mapato kwa masharti ya makubaliano na Marekani.

**"Wewe,Yako au mteja"** ina maana ni mtu anayeomba kufungua Akaunti au ambaye Akaunti imefunguliwa kwa jina lake, pamoja na chombo cha kisheria.

## 3. Uwasilishaji Vifaa na Uanzaji wa Kutumia Akaunti yako:

3.1 Iwapo tutaidhinisha maombi yako unaweza Kuitumia Akaunti yako kwa mujibu wa Masharti haya ikiwa maelekezo mengine yoyote yametekelezwa. Tutakuarifu kuhusu masharti hayo.

3.2 Tunaweza kukukabidhi vifaa vya matumizi ya Akaunti yako unapoifungua.

3.3 Tutakuarifu wakati ambapo kifaa kitakuwepo au kitakuwa tayari kuchukuliwa katika tawi lako.

3.4 Utaweza tu kutumia Akaunti yako utakapochukua kifaa chochote kinachotakiwa kwa ajili hiyo.

3.5 Unaweza kurejesha kifaa chochote ambacho hakifanyi kazi vizuri wakati wowote na tutakibadilisha.

## 4. Akaunti Yako

4.1 Una wajibu kuhakikisha Akaunti yako inahuishwa.

4.2 Unaweza kuomba kuweka ukomo wa utoaji wa fedha kwa siku au mwezi.

4.3 Hutaweza kutumia Akaunti yako kwa ajili ya kukinufaisha moja kwa moja au vinginevyo chombo kilichodhibitiwa.

4.4 Endapo tutashuku kwamba Akaunti yako imetumika kwa wizi, kizembe, kinyume na sheria, shughuli za utakatishaji pesa au kugharamia ugaidi na vitendo vinavyohusika nao, tunaweza:

4.4.1 kuzuia matumizi kwenye; au

4.4.2 kusitisha matumizi ya Akaunti yako mara moja bila taarifa kwako.

## 5. Taarifa ya Siri

5.1 Katika ibara hii ya 5, kumbukumbu kuhusu Taarifa ya Siri ina maana ya data zote, ripoti, kumbukumbu, nyaraka na taarifa yoyote iliyotayarishwa au kupatikana kuhusiana na maelezo haya.

5.2 Masharti ya ibara 5.1 kuhusiana na Taarifa ya Siri hayatumiki kwa:

5.2.1 taarifa ambayo inafahamika na umma; au

5.2.2 taarifa ambayo sheria au mahakama inatulazimisha kuitoa.

5.3 Isipokuwa kama ilivyoainishwa katika ibara hii ya 5, tutachukulia Taarifa ya Siri ya kila mtu kama siri na hatutatoa Taarifa ya Siri hiyo kwa mtu yeyote isipokuwa kama ilivyoelezwa katika ibara ya 5.

5.4 Unaridhia kwamba Benki itakuwa na haki ya kubadilishana Taarifa yako ya Siri ndani ya Kundi, ikibidi, kwa ajili ya Huduma kuhusiana na Akaunti.

5.5 Bila kujali chochote katika maelezo na masharti hayo, siku zote Benki itakuwa na haki ya kutoa Taarifa ya Siri yako kwa mtu mwingine. ikibidi, kwa ajili ya Utekelezaji mzuri wa Huduma kuhusiana na Akaunti.

5.6 Wajibu wa pamoja katika ibara hii ya 5 utaendelea kutumika hata baada ya kumalizika kwa maelezo na masharti haya na hutumii tena Huduma kuhusiana na Akaunti.

5.7 Unakubali kwamba Taarifa ya Siri haitatolewa kwa mtu mwingine yeyote isipokuwa aina ya watu wafuatao au katika mazingira maalum yafuatayo:

- 5.7.1 ikiwa Benki inalazimishwa kufanya hivyo chini ya Sheria yoyote ya Tanzania au ya kigeni kama inavyoweza kutumika mara kwa mara (pamoja, bila ya ukomo, FACTA au sheria kama hiyo katika mamlaka nyingine yoyote husika au sheria yoyote dhidi ya utakatishaji pesa na sheria yoyote ya ulinzi wa data);
- 5.7.2 kwa wadau wa Benki walioruhusiwa, washauri weledi, watoaji huduma au wakandarasi huru au mawakala wa wahusika walioruhusiwa kama mawakala wa kukusanya madeni, mashirika yanayochakata data na wanahabari ambao wana wajibu wa utunzaji siri kwa Benki au wahusika walioruhusiwa na Benki;
- 5.7.3 kwa mshirika yeyote halisi au mtarajiwa (mhusika ambaye anataka kuingia katika mkataba na sisi ambao unaweza kuathiri haki zako chini ya maelezo na masharti haya au mhawilishiwa (mtu ambaye haki au wajibu wetu wowote chini ya maelezo na masharti haya zinahawilishwa kisheria), au ofisa, muajiriwa, wakala au mshauri wa yeyote kati yao.
- 5.7.4 kwa mshirika yeyote wa biashara, mtoa bima au wakala wa bima, au mtoaji ulinzi wa mkopo moja kwa moja, au sio moja kwa moja, au wahusika/ wadau walioruhusiwa;
- 5.7.5 kwa taasisi ya kifedha yoyote ambayo una kazi nayo kwa madhumuni ya kukagua mikopo (pamoja na aina ya kumbukumbu za benki).
- 5.7.6 kwa mahakama, baraza au mamlaka yoyote (pamoja na mamlaka inayochunguza kosa) yenye mamlaka juu ya Benki na wewe;
- 5.7.7 kwa mdhibiti au mamlaka ya kodi ikiwa ni lazima kufahamu wajibu wowote wa kodi katika mamlaka yoyote kutokana na amri, mikataba na wadhibiti au mamlaka au vinginevyo;
- 5.7.8 kwa Benki Kuu ya Tanzania;
- 5.7.9 kwa mfanya biashara au mwanachama wa chama cha kadi ambapo utoaji huo unahusika na matumizi ya Kadi; na
- 5.7.10 kwa mtu yeyote aliye ruhusiwa au mtoaji ulinzi yeyote;
  - 5.7.10.1 kwa ajili ya kuzuia udanganyifu;
  - 5.7.10.2 iwapo utoaji ni kwa maslahi ya Benki;
  - 5.7.10.3 ikiwa utoaji unafanywa baada ya maombi yako au kwa ruhusa yako ya maandishi;
  - 5.7.10.4 ikiwa utoaji ni kwa ajili ya mslahi ya umma; na
  - 5.7.10.5 kwa yeyote ambaye tunaona ni lazima ili kukupatia Huduma kuhusiana na Akaunti, iwe ziko ndani au nje ya Tanzania.

5.8 Unakubali kwa wapokeaji wa taarifa tunazotoa, kutumia na kuhawilisha taarifa hiyo ikiwa ni lazima:

- 5.8.1 kukupatia wewe Huduma kuhusiana na Akaunti ;
- 5.8.2 kufuatilia utekelezaji wetu wa sheria, mikataba na mdhibiti yeyote, Mamlaka iliyoruhusiwa au wadau walioruhusiwa sera zetu, na sera za Kundi; au
- 5.8.3 kusaidia biashara yetu fedha na ufuatiliaji hatari, upangaji na ununuzi.

## 6. Maelezo kwenye Akaunti yako

6.1 Unaweza kutuomba maelezo ya Akaunti yako muda wowote katika tawi letu lolote na jukwaa la mtandao wa kielektroni.

6.2 Ikiwa unaamini kuna makosa katika maelezo ya Akaunti yako sharti utuandikie au utembelee tawi lako ndani ya siku thelathini (30) ya tarehe ya maelezo yenyewe.

6.3 Ikiwa hutatueleza kuhusu makosa yoyote ndani ya siku hizi thelathini (30) tutachukulia kwamba maelezo ya Akaunti yako ni sahihi.

## 7. Amana

7.1 Tutakubali uhawilishaji fedha kielektroni, uwekaji pesa na hundi katika Akaunti yako.

7.2 Malipo ya hundi na vitu vingine vinavyohusiana ambavyo vimewekwa vinaweza kutolewa kama pesa katika Benki ya mtoaji.

## 8. Kubadilisha Amana

8.1 Ikiwa sio mpokeaji halali wa fedha zilizoingizwa katika Akaunti yako tunaweza kutoa katika Akaunti na kumpa mpokeaji halali. Hata hivyo tutakueleza kama tumefanya hivyo.

**9. Malipo** Tutafanya malipo katika Akaunti yako ikiwa: unatuelekeza kufanya hivyo na kuna pesa za kutosha katika Akaunti yako.

## 10. Usitishaji malipo

10.1 Unaweza kusitisha malipo ya hundi ambayo umeitoa kabla haijahawisilishwa benki kwa malipo, isipokuwa kama tumethibitisha kwamba tutailipa.

10.2 Unaweza kukana na/au kusitisha malipo katika agizo la malipo kwa maandishi. Ni wajibu wako kumfahamisha mhusika ambaye atalipwa kwenye Akaunti yako.

10.3 Utaifidia Benki dhidi ya hatua ya kisheria inayotokana na ubatilishaji huo.

## 11. Kitabu cha hundi

Ikiwa unastahili kuwa na kitabu cha hundi unakubali kuchukua na kutumia kitabu cha hundi chochote na fomu zozote za hundi kwa uangalifu wa juu kabisa.

11.1 Aidha unakubali kuhakikisha:

11.1.1 kwamba fomu zote za hundi ambazo hazijatumika zinawekwa sehemu salama wakati wote;

11.1.2 kwamba tunajulishwa mara moja baada ya ugunduzi wako kuwa kitabu cha hundi chochote au fomu za hundi zozote zimeibwa, kupotea au kutoonekana;

11.1.3 kwamba mtu yeyote anayetayarisha hundi ameruhusiwa kufanya hivyo;

11.1.4 kwamba hundi yoyote inatayarishwa na kutiwa saini kwa wino au kifaa cha kuandikia kisichofutika;

11.1.5 kwamba kiasi kitakachoandikwa kwenye hundi kimeandikwa kwa umakini ili kuzuia maneno na herufi za ziada kujazwa bila kudhinishwa

11.1.6 kwamba kila hundi na marekebisho inatiwa saini na mtu aliyeidhinishwa.

11.1.7 kwamba hakuna hundi ambayo haijakamilishwa anapewa mgeni au mtu mwingine wakati huna sababu za maana za kuamini kwamba mtu huyo ni muaminifu;

11.1.8 kwamba baada ya ufungaji wa akaunti yoyote utaturejeshea fomu za hundi zozote ambazo hazijajazwa zilizobakia kuhusiana na akaunti hiyo na tutakurejeshea, inapowezekana, thamani ya stempu zozote za ushuru ambayo tumeipata.

11.2 unajua kwamba matumizi na uwekaji wa kitabu chako cha hundi ya inategemea mipango ambapo tunayo kuhusiana na utekelezaji wa mifumo ya MICR (Utambuzi wa Alama za wino wa Kimagneti) pamoja na ACH (Ofisi ya kushughulikia Hundi Kiautomatiki).

## 12. Ovadrafti

12.1 Ikiwa Akaunti yako inatolewa pesa zaidi bila mpango mzuri tunaweza kuhawilisha pesa kwenye akaunti hiyo kutoka akaunti nyingine ambazo unazo na sisi.

12.2 Ikiwa utashindwa mara moja kurejesha kiasi ambacho kimezidi tutakutoza riba kwenye kiasi hicho kilichotolewa kutoka tarehe ya ulipaji. Zaidi ya ulipaji. Zaidi ya tozo za riba, tutakutoza ada na tozo kama zilivyoainishwa katika jedwali la bei kama linavyorebishwa na

Stanbic Bank

Benki mara kwa mara.

12.3 Tunaweza kudai malipo yote kutoka kwako wakati wowote.

12.4 Cheti kilichotiwa saini na Meneja wa Benki chenye maelezo ya kina ya kiasi chochote, pamoja na riba, unachodaiwa itakuwa ni ushahidi wa kutosha isipokuwa ithibitishwe vinginevyo.

12.5 Ikiwa ni lazima, tunaweza kuchukua hatua za kisheria dhidi yako katika mahakama inayohusika.

12.6 Utawajibika kulipa gharama zote za kawaida katika kufidia kiasi unachodaiwa na sisi, pamoja na ada za kisheria kwa kiwango cha wakili na mteja, ada za ukusanyaji na utafutaji.

## 13. Akaunti ya Uwekezaji na Akiba

13.1 Zaidi ya Maelezo na Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma kwa akaunti ya uwekezaji wa kudumu au akaunti ya amana masharti yafuatayo yatatumika

13.2 Akaunti ya uwekezaji au amana ya kudumu haziwezi kuhawilishwa.

13.3 Kiwango cha riba ya akaunti ya uwekezaji wa kudumu kinaweza kurekebishwa na Benki mara kwa mara.

13.4 Kiwango cha amana ya Kudumu hakibadiliki mpaka amana inapokomaa.

13.5 Riba zote zitachukuliwa kwa kuvunjika kabla ya ukomavu kwa akaunti ya amana ya kudumu.

## 14. Utumiaji wa Kadi yako

14.1 **Masharti ya Jumla ya Kadi**

14.1.1 Zaidi ya Maelezo na Masharti Maalum ya Bidhaa na Huduma, masharti yafuatayo sharti yatumike kwa matumizi ya Kadi zako:

14.1.2 Sharti utie saini Kadi zako kwa wino wa kudumu unapozipokea. Tumia nafasi nyuma ya kadi yako.

14.1.3 Kadi hazitatumiwa kwa shughuli zozote haramu,

14.1.4 Daima tutakuwa ndio wamiliki wa Kadi.

14.1.5 Ikiwa utapoteza kadi yako sharti ulipie mpya.

14.1.6 Sharti utumie Kadi mwenyewe.

14.1.7 Huruhusiwi kuhawilisha Kadi yako kwa mtu mwingine yeyote.

14.1.8 Tutakupa PINI kukuwezesha kutumia Kadi yako.

14.1.9 Sharti ufuate kanuni za ubadilishaji fedha unapofanya miamala nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

14.1.10 Unaweza kutumia Kadi katika ATM yoyote, na kwa ajili ya miamala mingine unaweza kutumia Kadi yako katika ATM ambazo sio za Stanbic lakini utalipia ada ya ziada kwa kutumia mashine hizo.

14.2 Amana katika ATM na utoaji pesa ulizoweka

14.2.1 Unaweza kuweka pesa kwenye ATM na CDM za Benki ya Stanbic pekee.

14.2.2 Pesa uliyoweka kwenye ATM ya Benki ya Stanbic yoyote itajionyesha mara moja katika Akaunti yako.

## 15. Ada, riba, ukomo na uwekaji bei

15.1 Taarifa kuhusu tozo(ada, kodi, ushuru, faini na mfano wake) ambazo hutumia kuhusiana na Bidhaa na Huduma zetu iko katika brosha letu la ada linalopatikana katika brosha la bei ambalo tunachapisha na ni halali na kutumika kuanzia Januari 1 hadi Desemba 31 ya kila mwezi, isipokuwa tunapotoa taarifa tofauti.

15.2 Brosha letu la karibuni linapatikani kwako kutoka matawi yetu au kutoka tovoti yetu www.stanbicbank.co.tz

15.3 Tunaweza kupitia tozo zote kulingana na mzunguko wetu wa mapitio ya mwaka au wakati mwingine wowote kwa busara yetu.

15.4 Tutakutoza ada za ziada kwa utumiaji wa ATM ambayo sio yetu.

15.5 Viwango vyote vya riba vinawekwa kwa mwaka.

15.6 Hatutakutoza wewe riba zaidi kuliko inavyoruhusiwa na sheria.

15.7 Ambapo tunatakiwa kukulipa, riba inakokotolewa kwa salio la kila siku katika Akaunti yako na kulipwa kwa mwezi, au vinginevyo, kama tunavyokubaliana. Isipokuwa kwa akaunti ya akiba pekee, riba yoyote tunayolipa inahusika na kodi ambayo ipo.

15.8 Hatutakulipa riba katika akaunti yoyote mpaka malipo hayo yameainishwa kama kipengele cha Bidhaa maalum. Kufuatana na Masharti maalum ya Bidhaa/ Huduma zetu, tunaweza kubadilisha viwango vya riba

tunachokulipa kwa busara yetu na mabadiliko yoyote yanaweza kuanza kutumika baada ya taarifa ya siku thelathini (30).

**15.9 Utawajibika kwa ada zote, tozo, kodi/ ushuru na riba ambayo tunakutoza kwa mujibu wa Masharti haya na brocha ya karibuni mara kwa mara, pamoja na gharama za kupata fedha ambazo tunakudai. Hii ni pamoja na ada ya kisheria katika kiwango cha wakili na mteja, kamisheni ya ukusanyaji na ada za utafutaji.**

## 16. Ulinzi wa Data

16.1 Unatupa ridhaa kukusanya Taarifa yako Binafsi kutoka kwako na, iwapo ni halali na inafaa, kutoka vyanzo vya umma kuhusu mikopo, udanganyifu na madhumuni yaliyoainishwa hapa chini.

16.2 Unathibitisha kwamba,iwapo utatupa Taarifa Binafsi kuhusu au kwa niaba ya watu wengine (pamoja) na wenye saini katika akaunti, wenye hisa, maafisa watendaji wakuu, wadhamini na wanufaishwa) unaruhusiwa (a) kutuupatia Taarifa zao Binafsi kwa niaba yao; na hususan upelekaji wa taarifa nje ya mipaka kuhusu Taarifa Binafsi kwa na kutoka nchi ambako bidhaa na huduma vinatolewa; na (c) kupokea Taarifa Binafsi zote kwa niaba yao.

16.3 Unatupa ridha ya kutumia Taarifa Binafsi yako:

16.3.1 kwa ajili ya kukupatia bidhaa na huduma kwa mujibu wa Mkataba huu na kukupatia bidhaa nyingine na huduma unazoweza kuomba.

16.3.2 kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa kitakwimu na mwingine ili tuweze kutambua masoko muhimu na mwendo wake na kutathmini na kuboresha biashara yetu (hii inajumlisha kuboresha na kuendesha bidhaa na biashara mpya);

16.3.3 kwenye nchi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambako bidhaa na Huduma zinaweza zisiwe na Sheria sawa za ulinzi wa data kama nchi ambayo bidhaa na huduma zinatolewa. Tunapoweza, tutamuomba mhusika anayepokea kuafiki sera zetu binafsi;

16.3.4 kwa kutumia pamoja Taarifa Binafsi yako na watoaji wetu huduma wengine, ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Tunaomba watu wanaotoa huduma kwetu kukubali sera zetu binafsi iwapo wanahitaji kutumia Taarifa Binafsi yoyote kufanya shughuli zao/na

16.3.5 Ndani ya Kundi.

16.3.6 Unatambua kwamba tunatakiwa na sheria mbalimabli kukusanya sehemu ya Taarifa yako Binafsi na unaridhia kutumia taarifa hii na sisi.

16.4 Utapata taratibu za utumiaji wetu katika maelezo ya Kundi na yetu binafsi.Maelezo haya yanapatikana katika tovoti ya Kundi au kwa maombi.

16.5 Ikiwa huna hakika na hali yako ya Kodi au kisheria kwa kuwa Taarifa yako Binafsi inatumija katika nchi mbalimbali na unayoishi, pata ushauri binafsi.

**16.6 Utafutaji Masoko**

16.6.1 Hapa unaridhia kwa Benki kutumia data na taarifa yako binafsi ndani ya kundi iwapo ni lazima kwa madhumuni ya utafutaji masoko na utoaji huduma kwako.

16.6.2 Tunaweza kutumia Taarifa Binafsi yako kukueleza kuhusu bidhaa, huduma na ofa maalum kutoka kwetu au kampuni ambazo zimeweza kukuvutia. Tutafanya hivi kupitia baruapepe, ujumbe wa maandishi (sms), mitandao ya jamii au kukuarifu kwenye maombi yako ya simu ya kiganjani. Ikiwa baadae unaona hutaki sisi kufanya hivi, tafadhali wasiliana nasi kupitia mtandao wetu wa huduma kwa wateja kusitisha huduma hii.

## 17. Utambulisho na udhibiti kuhusiana na udanganyifu

Tunaweza kufanya utambulisho na udhibiti kuhusiana na udanganyifu kwako na kubadilisha taarifa kuhusiana na maombi yako kwako mintaarafu Akaunti yako na uendeshaji wake kwa jumla na mamlaka

husika.

**18. Kubadilishana taarifa kuhusu tuhuma za mwenendo wa kihalifu**

Iwapo tunashuku kwamba Akaunti yako inatumika kwa shughuli za kihalifu, tunaweza pia kutoa taarifa za undani kuhusu Akaunti na mawasiliano yako pamoja na undani wa mwenendo wa Akaunti yako vilivyosababisha tuhuma yetu kwa mamlaka husika.

**19. Mikopo na udhibiti husika**

Tunaweza kuchunguza kuhusu hali yako ya kifedha wakati wowote na sharti utupatie taarifa yoyote ya kifedha au taarifa muhimu ambayo tunaweza kuiulizia mara kwa mara.

19.1 Tunaweza kuchunguza mwenendo wako wa malipo na mawakala wa taarifa na mikopo wowote au mhusika yeyote

19.2 Tunaweza kuwapatia mawakala wa taarifa za mikopo taarifa sahihi kuhusu uendeshaji wa Akaunti yako pamoja na kushindwa kwako kutekeleza masharti haya.

19.3 Tunaweza kuzipatia benki nyingine, baada ya kuombwa, taarifa za benki kuhusu mwenendo wa Akaunti yako

**20. Kukatisha uhusiano wako na sisi**

20.1 Huwezi kuachia au kuhawilisha haki zako zozote au wajibu katika Mkataba huu bila idhini yetu ya maandishi kwanza.

20.2 Ikiwa umeamua kufunga Akaunti yako sharti uende kwenye tawi lako na ithibati ya utambulisho wako.

20.3 Ikiwa unafunga Akaunti yako sharti iwe imefuata sheria zote kabla ya kutoa pesa kutoka Akaunti hiyo.

20.4 Tunaweza kufunga Akaunti yako kwa kutoa kwako taarifa ya maandishi ya siku thelathini (Taarifa ya Ukatishaji).

20.5 Hatuhitaji kukupa taarifa katika mazingira yafuatayo na tunaweza kufunga Akaunti yako mara moja katika mazingira yafuatayo, iwapo:

20.5.1 Tunaamini au kushuku kwamba inatumika kiudanganyifu, kizembe, kinyume na sheria, au kwa shughuli za utakatishaji pesa, au kufadhili shughuli za kigaidi au zinazohusiana nazo;

20.5.2 tunaamini au kushuku kwamba utumiaji wa Akaunti yako moja kwa moja au vinginevyo unanufaisha Chombo Kilichozuiwa;

20.5.3 tunaarifiwa kuwa ni chombo kilichozuiwa; au

20.5.4 sharti tufanye hivi kwa sababu nyingine za kisheria.

20.6 Ikiwa tutafunga Akaunti yako tunaweza kudai pesa yoyote tunayokudai. Sharti ulipe fedha zote tunazokudai kwa mujibu wa tarehe ambayo iko kwenye Taarifa ya Ukatishaji.

20.7 Tutakuarifu kwa maandishi kupitia mitandao yetu mbalimbali iwapo tunaamini kwamba hutumii tena Akaunti yako. Tutakupa fursa ya kuanza kutumia Akaunti yako tena ambapo tunaweza kuifunga endapo hutaanza kuitumia tena.

20.8 Ikiwa Akaunti imefungwa sharti ufanye yafuatayo mara moja:

**20.8.1 kata Kadi yako katika vipande vipande ili isiweze kutumika tena. Iwapo hutaitakata Kadi yako utawajibika kwa Miamala yote ya kadi baada ya kufungwa kwa Akaunti yako; na**

**20.8.2 haribu hundi zote ambazo hazijatumika ili zisiweze kutumika tena. Ikiwa hutaharibu hundi ambazo hazikutumiwa hatutawajibika kwa upoteaji au hasara anayoipata mtu yeyote iwapo hundi hizi zitatumika kwa udanganyifu.**

**21. Kipindi cha Mpito**

21.1 Sehemu hii ya 21 inatumika tu iwapo unatoa kadimisho la kuwa na mkataba nasi, au kuwa na mkataba nasi kama mlaji, yaani kama mtu binafsi unayeshughulika kwa ujumla au kiasi kikubwa nje ya ujuzi, biashara, sanaa au weledi wako.

21.2 Unaweza kuondoa kadimisho la kuingia katika mkataba nasi; au kukatisha mkataba ulioingia nasi wakati wowote ndani ya muda huo:

(a) kuanzia wakati wa uwasilishaji wa kadimisho lako; na pia itaendeshwa na sera na taratibu zetu.

(b) kuishia mwisho wa siku kumi za kazi baada ya siku ambayo mkataba umeanza, kwa mujibu wa ibara 21.3 hapa chini. Huna haja ya kutoa sababu yoyote ya uondoaji au ukatishaji huo.

21.3 Unaridhia kwamba tunaweza kuanza kutoa huduma kabla ya kuisha kwa muda uliorejewa katika ibara ya 21.2 hapo juu, na unakiri kwamba iwapo tutaanza kutoa huduma kabla ya mwisho ya muda huo basi:

(a) ikiwa huduma zitatekelezwa kwa ukamilifu, utapoteza haki ya kukatisha iliyorejewa katika ibara ya 21.2 hapo juu;

(b) ikiwa huduma zitakuwa zimetolewa kiasi wakati wa ukatishaji sharti utulipe kiasi kinacholingana na huduma zilizotolewa au tunaweza kutoa kiasi hicho kutoka kwenye marejesho unayostahili kwa mujibu wa ibara ya 21.

21.4 Ili uweze kuondoa kadimisho la mkataba au kukatisha mkataba kwa sababu zilizoelezwa katika ibara ya 21, sharti utuarifu kuhusu uamuzi wako wa kujitoa au kukatisha (kulingana na hali yenyewe). Unaweza kutuarifu kwa njia yoyote ya maelezo ya wazi kuhusu uamuzi huo. Kuhusiana na ukatishaji unaweza kutuarifu kwa kutumia fomu ya ukatishaji ambayo tutakupatia. Ili uwe ndani ya muda wa ukatishaji, inatosha kwako, kutuma mawasiliano kuhusiana na utekelezaji wa haki ya kukatisha kabla ya kipindi cha ukatishaji kumalizika.

21.5 Ikiwa unaondoa kadimisho la kufanya mkataba, au kukatisha mkataba kwa sababu zilizoainishwa katika ibara ya 21, utarejeshewa kiasi chote ulichotulipa kuhusiana na kadimisho au mkataba isipokuwa kama ilivyoainishwa katika ibara ya 21.

21.6 Tutarejesha fedha kwa kutumia njia iliyotumika kufanya malipo isipokuwa kama umekubaliana vinginevyo kwa uwazi. Kwa vyovyote hutatozwa ada zozote kutokana na urejeshashaji huo.

21.7 Tutatayarisha marejesho unayostahili kutokana na ukatishaji kwa sababu zilizoainishwa katika kifungu cha 21 bila ya kuchelewa na, kwa vyovyote vile, ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya siku ambayo tumearifiwa kuhusu ukatishaji.

## 22. Anuani za Taarifa

22.1 Anuani ya mtaa wako kwenye fomu ya maombi ndio anuani uliyochagua kwa kupokelea taarifa na hati zozote za kisheria. Sharti utuandikie mara moja iwapo anuani yako itabadilika.

22.2 Tunaweza kuamua kutunza taarifa ambazo sio za kisheria kuhusiana na Akaunti yako kwenye anuani ya barua pepe yako, kama ipo, unayoitoa kwenye fomu ya maombi au kwenye anuani ya posta unayoitoa kwenye fomu ya maombi yako.

22.3 Tutachukulia kuwa umepokea taarifa yoyote tunayoituma kwako ndani ya siku kumi na nne baada ya kuposti, au siku ile ile iwapo itatumwa kwa mkono au kwa barua pepe.

22.4 Sharti utuarifu mara moja kuhusu mabadiliko yoyote ya anuani.

22.5 Tunachagua kuwa anuani yetu kwa ajili ya mienendo ya taarifa za kisheria ambapo michakato na taarifa zinazohusiana au kutokana na Mkataba huu, ukiukaji au uvunjwaji wake inaweza kutumwa au kuletwa kwetu, kama:

**Benki ya Stanbic Tanzania**
Kiwanja Na. 99 A
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/Barabara ya Kinondoni
SLP 72647
Dar es Salaam

## 23. Utekelezaji

23.1 Tunatakiwa na sheria kuomba taarifa fulani kukuhusu na watu wengine wanaokuhusu au kuhusiana na wewe na kuhakikisha taarifa hiyo na nyaraka ambazo tutaomba kutoka kwako ikiwa tutaamini ni muhimu au sahihi.

23.2 **Ikiwa hutatekeleza maombi yetu au ukiwa hutupi taarifa au nyaraka tunaweza kukataa maombi yoyote uliyoyaleta kwetu au tunaweza kufunga Akaunti yako mara moja.**

23.3 **Ikiwa wakati wowote tunashuku kuwa Akaunti yako hailingani na sheria, tunaweza kuzuia miamala kuanzishwa au kutekelezwa mpaka Akaunti yako ifuate sheria kikamilifu.**

**24. Jumla**

24.1 Tunaweza kubadilisha Masharti haya wakati wowote kwa kutoa taarifa ya maandishi kwako kwa kutumia njia mbalimbali kama (SMS) barua pepe, barua, taarifa kwenye ATM, ndani ya matawi yetu na njia yoyote ambayo tutaona muhimu mara kwa mara.

24.2 Mabadiliko hayatakatisha mkataba huu.

24.3 Huwezi kubadilisha vipengele vyovyote vya Masharti haya.

24.4 Masharti maalumu ya Bidhaa/Huduma yatatumika iwapo kuna mgongano baina yake na Masharti ya waraka huu.

24.5 Masharti haya yanasimamiwa na Sheria ya Tanzania.

24.6 Unakubali kuwa mahakama yenye mamlaka Kamili na Benki, ikipenda, kuweza kuchukua hatua za kisheria kutekeleza haki yoyote ya Benki.

24.7 Upendeleo au nafuu tunayoweza kukuruhusu havitaathiri au kubadilisha haki zetu zozote dhidi yako.

24.8 Iwapo unatudai fedha, hati iliyotiwa saini na meneja wetu yeyote kueleza kwamba:

24.8.1 ukweli kwamba deni linatakiwa kulipwa;

24.8.2 kiasi cha kulipwa;

24.8.3 riba inayohusika; na

24.8.4 tarehe ya kuanzia kukokotoa riba, itakuwa ni uthibitisho tosha wa maelezo yaliyotolewa kwenye hati, isipokuwa unapoweza kuthibitisha vinginevyo. Sio lazima kuthibitisha kuajiriwa kwa meneja aliyetia saini hati.

24.9 Lazima utuandikie mara moja endapo mazingira yako yanabadilika au yanaweza kusababisha hatari kwetu.

24.10 Kutotumika, ubatili au kutotekelezeka kwa ibara yoyote ya Masharti haya maalumu ya Bidhaa/Huduma hakutaathiri utumikaji, uhalali au utekelezaji wa ibara nyingine za Masharti haya au Masharti Maalum ya Bidhaa/Huduma yoyote.

**25. Kuondolewa kwa majukumu yetu kwako**

**25.1 Sisi (pamoja na mtu yeyote ambaye tunawajibika kwake) hatutawajibika kwa hasara yoyote (pamoja na zile zilizoelezwa katika ibara ya 25.2 hapa chini) kutokana na:**

**25.1.1 kufungwa kwa au kusitishwa matumizi kwa au kuzuiwa kwa shughuli zozote kwenye Akaunti yako na sisi kwa sababu yoyote;**

**25.1.2 kutekeleza kwetu Sheria zozote;**

**25.1.3 mazingira yoyote nje ya uwezo wetu kama vile (bila ukomo) majanga ya asili yasiyozuilika katika utendaji, migomo, au migogoro ya kikazi, vurugu, ghasia za kiraia au fujo, makatazo yoyote yaliyowekwa ( au hatua iliyochukuliwa) na Mamlaka ya Uwekezaji Vikwazo, mamlaka ya kiserikali au kisheria au mtu mwingine yeyote; kuingiliwa kokote kwa Huduma, ucheleweshaji, kukatika kwa umeme, kuharibika kwa kifaa chochote, kituo cha data za kielektroni, ATM, mtandao au mfumo mwingine. Tutakuarifu mapema kupitia njia mbalimbali, hii ni pamoja lakini sio pekee, ujumbe mfupi wa simu, barua pepe, barua, taarifa kwenye ATM, kwenye matawi yetu na njia nyingine ambazo tutaona muhimu mara kwa mara.**

**25.2 Masharti ya ibara ya 25.1 yanajumlisha madai kwenye mkataba, tendo au sheria kwa adhabu dhahiri au la ; hasara**

**inayosababishwa au mahususi pamoja na ukosaji wa faida.**

## 26. Sheria ya Utekelezaji wa Akaunti za Kigeni

26.1 Unaelewa kuwa kama sehemu ya majukumu ya Benki kutekeleza FATCA, tunatakiwa kupata taarifa kuhusiana na kodi yako kuamua iwapo Akaunti yako ni ya Marekani, Akaunti ya Mmiliki Mkorofi au Taasisi ya Fedha ya Kigeni isio Mshirika.

26.2 Unaipa Benki ridhaa ya:

26.2.1 kupata kutoka kwako taarifa kuhusu kodi kadiri inavyohitajika na katika muundo ulioamuliwa na Benki kuamua iwapo unaangukia katika kundi lolote la hapo juu, ambapo data za asili yako na miamala mtambuka kama inavyoamuliwa mara kwa mara na US IRS, itawasilishwa na Benki kwa IRS;

26.2.2 kwa Mawakala wa Uzuiaji ikiwa na wakati itatakiwa chini ya kanuni za FATCA; kuzuia malipo yoyote ya vyanzo vya Mapato ya Marekani yaliyopokelewa na wewe kwa kiwango ambacho hakijawahi kufanywa na Wakala wa Uzuiaji yeyote (zingatia kwamba uzuiaji wa juu unaoweza kutumika kwa vyanzo vya mapato vya Marekani chini FACTA ni asilimia 30); na

26.2.3 kufunga, kuzuia au kuhamisha (kwa moja ya vyombo vyetu vinavyohusika) Akaunti yako ndani ya siku tisini (90) kwa taarifa yako kuhusiana na kodi (kwa muundo utakaoamuliwa na sisi).

26.2.4 Hata hivyo tafadhali tambua kwamba Benki sio mshauri wa kodi na haitoi ushauri wowote wa kiweledi wa kodi kuhusiana na FACTA au sheria nyingine yoyote ya kodi. Unahamasishwa kupata ushauri wa kiweledi huria kuhusu FACTA na mambo mengine yoyote kuhusiana na kodi.

## 27. Fedha

27.1 Fedha yoyote iliyopokewa na Benki, kwa fedha tofauti na ya Akaunti, inaweza kubadilishwa na Benki kuwa fedha ya Akaunti au fedha nyingine kadiri ambavyo Benki inaona ni lazima kufidia majukumu au madeni yako. Benki itatumia kiwango cha kubadilisha fedha kwa ajili ya mabadiliko hayo.

27.2 Endapo yatatokea mabadiliko makubwa katika mazingira ya soko yatakayoathiri uwezo wa Benki kutoa au kulipa mkopo kwa fedha za kigeni, Benki inabaki na haki kwa hiari yake yenyewe, kubadilisha deni lako la fedha ya kigeni kuwa fedha ya Tanzania kwa kutumia kiwango cha siku hiyo ya ubadilishaji.

27.3 Endapo Benki itadai malipo yoyote ya deni lako, baada ya madai hayo kufanyika, Benki ina haki, kwa hiari yake yenyewe, kubadilisha deni lako lolote la fedha ya kigeni kuwa fedha za Tanzania kwa kiwango cha kubadilisha fedha kwa siku ya ubadilishaji.

27.4 Katika kutumia haki hizo zilizotajwa ya kubadilisha deni la fedha ya kigeni kuwa Shillingi ya Tanzania, benki haitawajibika kwa hasara yoyote kutokana na mabadiliko ya kiwango cha fedha za kigeni.

## 28. Makato Deni

28.1 Kutokana na sisi kukupatia fedha na/au nyenzo nyingine, unakubali kwamba kwa nyongeza nyingine yoyote ya deni la jumla (haki ya Benki ya kuzuia mali ya Muwekaji) au haki kama hiyo ambayo sisi kama Benki tunaweza kuruhusiwa na Sheria, tunaweza wakati wowote na bila taarifa kwako kuunganisha yote au yoyote kati ya Akaunti zako pamoja/na dhima kwetu na kata deni au hawilisha kiasi chochote au

kiasi kinachodaiwa katika Akaunti yoyote au Akaunti hizo kwa ajili ya kulipa madeni yako kwetu kwenye Akaunti nyingine yoyote au kwa namna nyingine yoyote, madeni hayo yawe halisi au tegemezi (kutegemea utokeaji wa jambo jingine) la msingi au pamoja au tofauti au kwa pamoja. Benki itamjulisha Mkopaji baada ya ukamilishaji wa mkato wa deni.

**29. Benki Isio na Mipaka**

Kwa madhumuni ya kibenki katika Akaunti yako katika nchi za kigeni zilizochaguliwa, kadiri tutakavyokushauri mara kwa mara, iwe pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, unakiri na kukubali kwamba:

29.1 Tafsiri za "sisi", "yetu", na Benki" inahusisha washirika wetu katika nchi inayotumia au kuhodhi fedha ya kigeni inayohusika;

29.2 fedha itakayotolewa itakuwa fedha inayopatikana katika kaunta za utendaji;

29.3 upatikanaji wa huduma utategemea saa za kazi za kawaida katika nchi ambayo unafanya utendaji;

29.4 upatikanaji wa huduma utategemea miamala ya kaunta;

29.5 Benki inaweza, kwa hiari yake pekee, kuweka ukomo kwa muamala kwa siku kwa miamala iliyokamilika nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Benki itakushauri kuhusu ukomo, kama inahusika, mara kwa mara.

**30. Akuanti za Pamoja**

30.1 Utaipatia Benki, katika fomu za kukubali, saini za kielelezo ya kila mtu aliyeidhinishwa kutumia Akaunti.

30.2 Isipokuwa kama imekubalika vinginevyo, watia saini wote wana uwezo wa kutoa yote au sehemu ya mali au dhamana inayowekwa na Benki mara kwa mara, kufungua Akaunti ya ziada kwa jina lako na kutoa zaidi kati ya Akaunti zako zozote. Endapo wateja wawili au zaidi wana Akaunti ya pamoja dhima yote ni ya pamoja na kadhaa.

**31. Miongozo ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni**

31.1 Benki inategemea matakwa ya miongozo kuhusu ubadilishaji fedha za kigeni, inayotolewa na Benki Kuu mara kwa mara.

31.2 Katika utekelezaji miongozo husika kwenye ubadilishaji fedha za kigeni, Benki itatakiwa kukusanya taarifa ya ziada kutoka kwako mintarafu miamala ya ubadilishaji fedha za kigeni (Fx) zaidi ya sawa na Dola za Kimarekani (USD) 10,000. Unakubali hapa kutoa nyaraka ziada za uthibitisho na Benki na/au mamlaka ya udhibiti husika.

**32. Ufungaji/Usitishwaji wa matumizi ya Akaunti**

Benki inaweza wakati wowote kusitisha matumizi au kufunga Akaunti ikiwa kuna mgogoro au ikiwa benki ina shaka ya maana kutokana na sababu yoyote kuhusu mtu au watu wanaostahiki kuiendesha au baada ya kupokea amri ya mahakama au maelekezo yaliyotolewa na chombo chenye Mamlaka au Chombo kinachohusika. Benki haitalazimika kufungua shauri la kudaianisha (shauri linalofunguliwa na mhusika wa tatu kuyaomba mahakama yaamue haki za umiliki kati ya wadaawa wawili kuhusu pesa au mali moja) au kuchukua hatua yake yenyewe ya uamuzi wa mgogoro au wasiwasi huo.

**33. Utulivu**

Endapo Akaunti yako ni tulivu kwa muda ulioainishwa kama ilivyowekwa na sera na taratibu za Benki, Benki inaweza kufunga Akaunti baada ya kukupatia taarifa ya kusudio la kufanya hivyo na kukueleza sababu ya kufanya hivyo . Fedha zozote ambazo zimezuiwa katika Akaunti wakati wa ufungaji zitalipwa kwako au wakala wako wa sheria. Wakati wa kipindi cha taarifa, unaweza kuchukua hatua kuihuisha Akaunti, na endapo itafanyika kwa ridhaa ya Benki, Akaunti haitafungwa.

**34. Malalamiko ya Wateja**

34.1 Ili kuifanya iwe rahisi kadiri inavyowezekana zifuatazo ni njia za kutuma malalamiko yako kuhakikisha kwamba yamesikilizwa:

34.1.1 Tembelea moja ya Benki zetu na kuzungumza na mfanyakazi wake;

34.1.2 Tuma malalamiko yako kwa mtandao kwa: tanzaniaccc@stanbic.com;

Stanbic Bank

34.1.3 Piga Kituo cha Kuwasiliana na Wateja laini ya bure **Na. 0800 751111** au; Weka malalamiko yako kwa maandishi na tuma kwa:

**Meneja wa Huduma Benki Binafsi (PPB)**
Benki ya Stanbic
Makao Makuu
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/Barabara ya Kinondoni
SLP 72647 Dar es Salaam

34.2 Endapo malalamiko yako hayatatatuliwa ndani ya siku ishirini na moja (21) (au muda uliokubaliwa) au iwapo hukuridhika na matokeo ya mchakato ulioanishwa na ibara ya 34.1 hapo juu, unaweza kupeleka malalamiko mbali zaidi kwa kutuma barua pepe kwa tanzaniacccescallations@stanbic.com au andika kwa:

**Mkuu wa Huduma**
Benki ya Stanbic
Makao Makuu
Kona ya Ali hassan Mwinyi Barabara ya Kinondoni
S.L.P 72647 Dar es Salaam

34.3 Ikiwa malalamiko yako hayatatatuliwa ndani ya kipindi cha kutatua malalamiko ya mteja kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Benki ya Tanzania kuhusu Kinga ya Watumiaji Fedha kama ilivyorekebishwa mara kwa mara, unaweza kupeleka malalamiko yako kwa maandishi Benki Kuu ya Tanzania:

**Dawati la Kutatua Malalamiko**
Ofisi ya Katibu wa Benki
2 Mtaa wa Mirambo
SLP 11884
Dar es Salaam